MAADILI MUHIMU

UKRISTO

UTAKATIFU

UMISHENI

UKRISTO
UTAKATIFU
UMISHENI

Christian
Holiness
Missional

Kiswahili

Re-printed with Permission by
Africa Nazarene Publications
P O Box 1288 Florida 1710
Republic of South Africa

ISBN-978-0-7977-1182-2

Imani Iliyo Hai:
Imani Ya Wanazareti

Kila shirika linalodumu kwa muda mrefu misingi yake huwa ndani ya mkusanyiko wa ushirikiano wa kusudi, imani na maadili. Hivyo ndivyo ilivyo katika Kanisa la Mnazareti. Kanisa la Mnazareti lilianzishwa ili kubadilisha ulimwengu kwa kueneza maandiko ya utakatifu. Hili ni Kanisa la Ujumbe Mkuu na la Utakatifu. Huduma yetu ni kuwafanya wanafunzi wanaofanana na Kristo katika mataifa yote.

Maisha ya sasa na yale ya siku zijazo ya Kanisa la Mnazareti yanaelezwa kwa kushiriki katika huduma ya Mungu. Kwa hivyo hii ni sauti ya Kanisa la Yesu Kristo na shirika lililo la kipekee, sio katika imani yake ila pia kwa njia ya kipekee inavyochangia katika ufalme wa Mungu.

Kanisa la Mnazareti linapoingia katika milenia mpya, ni vyema kutambua vitu vya kipekee tunavyofurahia, kukumbatia na kusherehekea. Mambo ya thamana zaidi kwetu ni – huduma yetu, wito, imani na maadili. Haya ni mambo tunayotea kama zawadi kwa vizazi vijavyo.

Ni ombi letu kuwa maadili yetu muhimu yataendelea kuhudumu kama mwongozo wa mwanga kwa wale wanaojaribu kupitia kwa nuru na kivuli cha karne zijazo.

MAADILI MUHIMU

1. Sisi ni Wakristo

Kama washiriki wa Kanisa la Kimataifa, tunaungana na waumini wengine wote katika kukiri kuwa Yesu Kristo ni Bwana na katika kupokea kanuni za imani ya Ukristo. Tunathamini urithi wetu wa Utakatifu –wa Wesleyan, tunaamini kuwa hii ndiyo njia ya kuelewa imani iliyo kweli kwa Maandiko, sababu, mila na uzoefu.

2. Sisi ni Watu Watakatifu

Mungu, ambaye ni mtakatifu, anatuita katika maisha ya utakatifu. Tunaamini kuwa Roho Mtakatifu anatafuta kutufanyia kazi ya neema kwa mara ya pili, ambao kwa majina mengine tunazifahamu kama "utakaso kamili" na "kubatizwa kwa Roho Mtakatifu" – kututakasa kutoka kwa dhambi; kutufanya upya kwa mfano wa Mungu; kutuongeza nguvu za kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote, moyo akili na nguvu, na kupenda jirani zetu kama nafsi zetu. Utakatifu katika maisha ya Wakristo kwa urahisi ueleweka kama kufanana na Kristo.

3. Sisi ni watu wa umisheni

Sisi ni watu "waliotumwa," tunaoitikia wito wa Kristo na wajazwa kwa Roho Mtakatifu ili kwenda ulimwenguni kote, kushuhudia Ukuu wa Kristo na kushirikiana na Mungu katika ujenzi wa Kanisa na katika uendelezaji wa Ufalme wake (2 Wakorintho 6:1). Misheni yetu (a) huanza katika ibada, (b)

kuhubiria ulimwengu katika uinjilisti na huruma, (c) kuwahimiza waumini katika kukua Kikristo kupitia kwa njia za uwanafunzi, na (d) kuwatayarisha wanawake na waume kwa huduma ya Ukristo kupitia kwa njia ya elimu ya juu.

Simulizi

1 Sisi ni Watu Wakristo

Tunaungana na waumini wengine wote katika kukiri Ukuu wa Yesu Kristo. Tunaamini katika upendo mtakatifu, Mungu ametoa msamaha wa dhambi kwa watu wote, na kurejesha uhusiano. Katika kupatanishwa na Mungu, tunaamini kuwa tunapatanishwa na kila mmoja, kupendana kama vile tulivyopendwa na Mungu, kusameana kama tulivyosamehewa na Mungu. Tunaamini kuwa maisha yetu pamoja ni mfano wa tabia za Kristo. Tunasimama pamoja na Wakristo wengine kila sehemu katika kukubali historia ya kanuni za imani na imani ya Wakristo na tunathamini urithi wa tamaduni za utakatifu wa Wesleyani.

Kati ya watu wote wa Mungu tunakiri na kumsifu Yesu Kristo kama Bwana.

Yesu Kristo ni Bwana wa Kanisa, kama vile Imani ya Mitume inavyotueleza, ni moja takatifu, shirika na la mitume. Katika Yesu Kristo na kupitia kwa Roho Mtakatifu, Mungu Baba ametoa msamaha wa dhambi na mapatano kwa ulimwengu wote. Wanaokubali wito wa Mungu kwa imani hufanywa wana wa Mungu. Baada ya kusamehewa na kupatanishwa katika Kristo, sisi pia tunasemehe na kupatana na kila mmoja. Katika njia hii, sisi ni Kanisa la Kristo na Mwili, na basi tunadhihirisha Mwili huo. Kama mwili mmoja wa Kristo, tunanye, “Bwana

mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. “Tunakubali umoja wa Kanisa la Kristo kuyashinda yote ili kuuvumilia (Waefeso 4:5, 3)

Yesu Kristo ni Bwana mtakatifu. Kwa sababu hii, Kanisa la Kristo sio moja tu lakini pia ni takatifu. Linapaswa kuwa takatifu katika sehemu zake zote na kikamilifu, takatifu katika washiriki wake kwa vile yeye ndiye Kichwa. Kanisa ni takatifu na limeitwa ili kuwa takatifu. Kanisa ni takatifu kwa sababu ni Mwili wa Kristo, ambaye amekuwa kwetu haki na utakatifu. Kitendo hiki kinafahamika kama kuwa mtakatifu kwa njia ya Mungu, ambaye alituchagua hata kabla ya misingi ya ulimwengu ili tuwe watakatifu na bila dosari. Kama mwili mmoja wa Kristo, maisha yetu pamoja kama kanisa inapaswa kubeba tabia takatifu za Kristo, ambaye alijitoa binafsi na kuchukua umbo wa mtumwa. Tunakubali utakatifu wa kanisa la Kristo, kama kipawa na wito.

Yesu Kristo ni Bwana wa Kanisa. Kwa sababu hii, Kanisa sio moja pekee na takatifu ila Umoja. Inajumlisha wale wote ambao hukubali maadili ya Imani ya Ukristo. Tunakubali imani ya mitume ambayo imeshikiliwa na Wakristo wote kila mahali, wakati wote. Tunalikumbatia wazo ya John Wesley la Roho wa umoja, ambamo tunao ushirika na watu wote wanaoamini maandiko muhimu, na hata pia tunawakubali wale ambao hawakubaliani nasi katika mambo ambayo sio muhimu katika wokovu.

Yesu Kristo ni Bwana wa maandiko. Kwa sababu hii, Kanisa sio moja takatifu na la umoja lakini pia ni la kitume. Limejengwa katika misingi ya mitume na manabii na huendela kujitolea katika mafundisho ya kitume. Kanisa hasa huangalia maandiko, ambayo ni ndiyo pekee aina ya

imani na maisha. Ukuu wa Yesu juu ya maandiko inamaanisha tunapaswa kuelewa maandiko kupitia kwa ushuhuda wa Roho Mtakatifu jinsi wanavyokiri Kristo. Ili kukubali na kurekebisha kuelewa kwetu kwa maandiko, tunapaswa kusikiza imani za kale na sauti zingine za tamaduni ya Ukristo ambayo kwa uaminifu hueleza maandiko. Sisi pia tunaruhusu kuelewa kwetu kuongozwe na sauti ya Roho Mtakatifu anayezungumza nasi katika toba, imani, uhakikisho. Mwishowe tunajaribu kuelewa kwetu kwa maandiko kwa kutafuta uwazi na maana ya ushuhuda wao kwa Yesu Kristo.

Sisi tumeitwa hasa ili kushuhudia utakatifu wa Kanisa la Kristo kama ilivyofundishwa katika tamaduni za Utakatifu wa Uwesleya. Tunazidhibitisha kanuni za wokovu kwa neema pekee kupitia katika imani ya Yesu Kristo Mwokozi wetu. Kwa matendo haya tunaendelea kuthibitisha kanisa la Kristo ni moja, la umoja na la kitume. Lakini wito wetu maalum ni kuungama mbele za macho ya ulimwengu na kanisa ambalo ni kiini cha utakatifu na kuwahimiza watu wa Mungu kuishi katika uwepo mtakatifu wa Baba. Kwa ajili ya sababu hii tunathibitisha kuelewa kwa imani ya Ukristo, na kutafuta kudumisha uaminifu katika kanuni za mafundisho. Neema ya Mungu tangulizi na njia ya neema, toba, imani, kuzaliwa mara ya pili, kuhesabiwa haki, uhuisho, jumuia la Wakristo na wanafunzi wake, na upendo dhabiti.

2 *Sisi ni Watu Watakatifu*

Tumeitwa na maandiko and kuvutiwa kwa neema ya kuabudu Mungu na kumpenda kwa mioyo yetu yote, akili na nguvu na kuwapenda jirani kama nafsi zetu. Tunajitolea nafsi zetu kikamilifu kwa Mungu, tukiamini kuwa tunaweza

kutakaswa kikamilifu," kama uzoefu wa pili. Tunaamini kuwa Roho Mtakatifu hufanya watu wahisi hatia, uwaosha, hujaza na kututia nguvu na neema ya Mungu hutubadilisha siku baada ya siku na kutufanya watu wa upendo wa Mungu na nidhamu ya kiroho, enye maadili mema, mienendo mizuri, huruma na haki. Ni kazi ya Roho Mtakatifu ambayo huturejesha katika mfano wa Mungu na kuzaa kwetu tabia ya Kristo. Utakatifu katika maisha ya Wakristo hueleweka vyema kama kufanana na Kristo.

Tunaamini katika Mungu Baba, muumba, anayeumba vitu vyote ambavyo havimo. Wakati mmoja hatukuwemo, lakini Mungu alituita na kutufanya wanadamu, alituumba kwa ajili yake na kwa mfano Wake. Tumeamriwa kubeba mfano wa Mungu: "Mimi ndimi Bwana wenu, jitakaseni mwe watakatifu kwa sababau min ni mtakatifu." (Mambo ya Walawi 11:4)

Njaa yetu ya kuwa watu Watakatifu inayo misingi ya Utakatifu katika Mungu binafsi. Utakatifu wa Mungu ni Uungu Wake. Uwepo wake pekee. Hakuna kama Yeye kwa ukuu na utukufu. Kwa mwanadamu ye yote katika uwepo huu analopaswa kufanya ni kuabudu Mungu kama Mungu. Utakatifu wa Mungu huonekana katika matendo yake ya wokovu. Kujiweka kwake Mungu anayedhihirisha na kujitoa nafsi huwezesha kuabudu, na ibada ndiyo njia ya msingi ya kumjua Yeye. Tunamwabudu Mungu mtakatifu, anayeokoa kwa kupenda kile anachopenda.

Ibada yetu kwa Mungu mkuu na mwenye neema huonekana katika njia nyingi. Mara ni katika maombi na sifa kwa imani ya jumuia. Wakati mwingine huonekana katika matendo ya kibinafsi ya ibada, kushukuru, kusifu na utiifu. Kushirikiana imani kwa Uinjilisti, kuonyesha

huruma kwa jirani zetu, kutenda haki, na tabia nzuri, yote ni matendo ya kuabudu mbele zake Mungu wa utakatifu unaowaka. Hata kazi za kawaida ni matendo ya kuabudu na huonyesha umuhimu kwa vile hufanya ibada ya Mungu mtakatifu kuwa njia yetu ya maisha.

Yesu Kristo alidhihirisha Mungu mmoja mtakatifu kwetu na kutuonyesha kuishi kwa utakatifu. Yesu anatufahamisha ili kuelewa utakatifu kupitia Maisha Yake, kafara na mafundisho kama yalivyo katika Injili, hasa mafundisho ya Mlimani. Kama Watu watakatifu, tunatafuta kufanana ya Yesu katika kila tabia na matendo. Kwa neema zake, Mungu huwawezesha Wakristo wanaomuabudu kwa mioyo yao yote kuisha kama Kristo. Tunaelewa hii kuwa msingi wa utakatifu.

Mungu pia ametupa kipaji na jukumu la kuchagua. Kwa sababu tulizaliwa aina ya kutenda dhambi, tunao uhuru wa kuchagua njia zetu badala ya njia za Mungu (Isaya 53:6). Kwa sababu ya kuleta uovu katika maumbile ya Mungu kwa dhambi zetu, tulikuwa wafu katika makosa na dhambi zetu (Waefeso 2:1). Ikiwa tutaishi tena kiroho, Mungu, ambaye huleta uhai kwa vitu ambavyo havimo, lazima kwa neema zake atuumbe tena upya kupitia kwa matendo ya wokovu ya Mwanaye.

Tunaamini kuwa Mungu aliingia ulimwenguni wetu kwa kufanya mwanadamu Mwana Wake wa Pekee. Yesu wa Nazareti, Mungu- mwanadamu katika historia. Yesu alikuja kufanya upya mfano wa Mungu ndani yetu, kutuwezesha kuwa watu watakatifu. Tunaamini kuwa utakatifu katika maisha ya Wakristo ni kwa sababu ya uzoefu wa dharura na mpango wa maisha marefu. Kufuatia vizazi, Roho wa Bwana hutuleta kwa neema

katika kujitolea kikamilifu Kwake. Hivi basi katika kitendo takatifu cha utakaso kamili, unaojulikana pia kama kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, Yeye hutusafisha kutoka kwa dhambi ya asili na kutuweka kwenye uwepo Wake Mtakatifu. Upendo wake ulio ndani yake, hutuwezesha kuishi kwa haki, na hutupa nguvu za huduma!

Roho wa Yesu hufanya kazi ndani yetu. Huzaa ndani yetu tabia zake za upendo mtakatifu. Hutuwezesha utu upya, ulioumbwa wa kufanana na Mungu kwa ukweli wa haki na utakatifu. (Waefeso 4:24) Kuwa kama Mungu ni kuwa kama Yesu. Baada ya kurejeshewa mfano mtakatifu katika kitendo cha Mungu cha utakaso kamili, tunakubali kuwa bado hatujafika Kiroho, lengo letu la maisha ni kufanana na Kristo katika kila neno, wazo na kitendo. Kwa kuendelea kuongezeka kwa, utiifu na imani, tunamini kuwa tunabadilishwa kwa mfano wake (Kristo) katika utukufu unaongezeka" (2 Wakorintho 3:18). Tunashiriki zaidi mpango huu tukiishi maisha ya ibada inayoonekana katika njia nyingi, kwa kupokea nidhamu ya kiroho, ushirika na uwajibikaji wa kanisa la mtaa. Kama mwili wa Wakristo katika shirika Fulani, tunataka kuwa jumuia linalofanana na Kristo, linaloabudu Mungu kwa moyo kamili na linalopokea vipawa Vyake vya pendo, safi, nguvu na huruma.

Kama Watu watakatifu hatuishi kwenye chumba cha historia. Tunatambua Agano Mpya na kanisa la kale. Kanuni zetu za imani zinatuweka vyema katika tamaduni Ukristo wa kipekee. Tunatambua tamaduni za Arminaini za neema ya bure (Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote na haki ya mwanadamu – uhuru tuliopewa na Mungu kwa wote wa kuchagua Mungu na Wokovu. Urithi wetu wa kanisa la Kikristo tunaupata katika Mfumo wa kuleta upya

wa Wesley wa karne ya 18 na katika Mfumo wa Utakatifu katika karne za 19 na 20.

Katika karne watu Watakatifu wamempenda Yesu kwa njia maalum. Tunaabudu Yesu! Tunampenda Yesu! Tunaongea juu ya Yesu! Tunaishi Yesu! Huu ndiyo msingi na ufurukaji wa utakatifu. Hii ndiyo tabia ya watu Watakatifu.

3 Sisi Ni Watu Wa Umisheni

3a. *Misheni yetu ya kuabudu*

Misheni ya kanisa ulimwenguni huanza kwa kuabudu. Sisi hukusanyika pamoja mbele zake Mungu kwa ibada - kwa njia ya kuimba, kusikiza masomo ya Biblia, kutoa fungu la kumi na sadaka, kuomba, kusikiza mahubiri, ubatizo na kushiriki meza ya Bwana – hivi tunajua wazi kabisa maana ya kuwa watu wa Mungu. Imani yetu kuwa kazi ya Mungu inakamilika kimsingi kupitia kwa ibada ya Wakristo hutuwezesha kuelewa kuwa misheni yetu inajumlisha zoezi kama vile kuwapokea wakristo wapya katika shirika la kanisa na kuwapanga ibada mpya kwa mashirika.

Ibada ni kuonyesha upendo wetu kwa Mungu. Ni heshima kuu kwa Yule Mmoja anayetuokoa kwa neema na huruma. Mwanzo wa ibada ni kanisa la mtaa mahali ambapo watu hukutana, sio kwa kujitukuza lakini kwa kujitoa kikamilifu kwa Mungu. Ibada ni kanisa katika kupenda, na kutii huduma za Mungu.

Ibada ni fursa na jukumu la kwanza la watu wake Mungu. Ni mkusanyiko wa jumuia la agano mbele zake

Mungu katika kukiri na kusheherekea Yeye ni Nani, Yale ambayo ametenda na Yale ambayo ameahidi kutenda.

Kanisa la mtaa liabudulo limo katikati ya kitambulisho chetu. Msingi wa kanisa la mnazareti ni ibada ya washirika wa mtaa, ni katika shirika hili na kupitia kwa shirika hili ndipo misheni yetu inapotimizwa. Misheni ya kanisa hupata maana na mafundisho katika ibada. Ni katika kuhubiri Neno, kusherehekea meza ya Bwana, kusoma maandiko katika umati, kuimba nyimbo na tambio, kuungana katika maombi, katika kutoa fungu letu la kumi na sadaka ndipo tunaelewa wazi maana ya kuwa watu wa Mungo. Katika ibada ndiko tunaelewa vyema zaidi maana ya kusirikia katika kazi ya Mungu ya wokovu.

Misheni yetu ya ibada ni msingi wa Kanisa letu. Kama ilivyo kwamba msingi wa kanisa la mnazareti ni ibada ya shirika la mtaa, misheni yetu ya ibadi itajumlisha kuendelea kujitolea katika kuanzisha mashirika mengine mapya.

3b. Misheni Yetu Ya Huruma na Uinjilisti

Kama watu waliowekwa wakfu kwa Mungu, tunashiriki katika upendo wake na huruma Yake kwa watu maskini na wale ambao wamevunjika. Amri Kuu na Utume Mkuu hutusongeza katika kushirikisha ulimwengu katika uinjilisti, huruma na haki. Hapa tunajitolea katika kuwaalika watu katika imani, kuwatunza wenye mahitaji, kusimama na wale wanaodhulumiwa, kufanya kazi katika kulinda na kuhifadhi maumbile ya kazi ya Mungu, na hata

kujumlisha katika ushirika wetu wote ambao wataliita jina la Bwana.

Kupitia kwa misheni yake ulimwenguni, kanisa laonyesha upendo wa Mungu. Hadithi ya Biblia ni hadithi ya upatanisho ya ulimwengu na Mungu, kupitia kwa Yesu Kristo (2 Wakorintho 5:16-21). Kanisa linatumwa ulimwenguni ili kushirikiana na Mungu katika huduma ya upendo na upatanisho kupitia kwa uinjilisti, huruma na haki.

Utume Mkuu na Amri Kuu ndizo nguzo za kutusaidia kuelewa misheni yetu. Ni semi mbili lakini misheni ni moja, pande mbili za ujumbe mmoja wa injili. Yesu anayetuagiza, “mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na ka akili zako zote. Hii ndio amri iliyo kuu, tena ya kwanza. Nayo ya pili ni kama hiyo, nayo mpende Jirani yako kama nafsi yako.” (Mathayo 22:37, 39), pia tunaelezwa, “kwa sababu hii, enendeni ulimwnguni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, Nanyi wafundisheni kuyashika mambo yote nilyowaamuru ninyi” (28:19-20)

Misheni ya Kanisa ulimwenguni inaenea kwa watu wote, kwasababu watu wote, wameumbwa kwa mfano wa Mungu, na dhamana yao ni kuu. Ni misheni yetu kuwapenda na kuwathamini watu kwasababu Mungu anawapenda na anawathamini. Mungu anawaletea amani, haki na wokovu kutokakwa dhami kupitia kwa Kristo. Ni misheni yetu kuwa wenye huruma na kuwatunza watu wenye mahitaji. Ni misheni yetu kupinga mambo yanayogandamiza watu.

Misheni ya Kanisa inaenea kwa kila mtu kikamilifu. Mungu ametuumba kikamilifu kwahivyo ni misheni yetu kuhubiri upendo wa Mungu kwa watu kikamilifu – mwili, moyo na roho. Misheni yetu ya uinjilisti, huruma na haki ni ujumbe mmoja lakini uliogawanywa. Unawashughulikia mahitaji ya watu ya mwili, hisia na kiroho.

Misheni ya kanisa ulimwenguni inaenea kwa watu wote kwasababu ya Roho Mtakatifu, aliwashukia watu wote wakati wa pentekosti. (Matendo ya Mitume 2) Ni misheni yetu kuwasilisha ujumbe wa wokovu kupitia kwa Yesu Kristo kwa kila mtu ulimwenguni. Tumejazwa na Roho ili kuenda ulimwenguni na kukiri Ufamle na kushirikiana na Mungu katika ujenzi wa Kanisa.

Kwa roho ya matumaini na matarajio ya matokeo mazuri ndipo tunashughulisha misheni yetu tuliyopewa na Mungu ulimwenguni. Kitendo hiki ni dhihirisho la kuonyesha jinsi mwanadamu anavyoshughulika. Misheni yetu ni kuitikia wito wa Mungu. Tunafanya hivi kwa kushiriki na Mungu katika misheni ya ufalme ya upatanisho. Ni ushuhuda wa uaminifu wa kanisa na upendo wa Mungu ulimwenguni katika uinjilisti, huruma na haki. Kwa imani katika uwezo wa neema ya Mungu ya kubadilisha maisha ya watu walivunjwa na dhambi na kuwarejasha kwa mfano Wake.

3c. **Misheni Yetu ni Uwanafunzi**

Tumejitolea katika kuwaalika watu wengine katika kufanywa wanafunzi wa Yesu. Kwa sababu tunafahamu hivi, tunajitolea katika kuwapa vifaa ambavyo vitawasaidia kufikia lengo hili. Vifaa hivi ni kama vile (shule ya jumapili,

Mafundisho ya Biblia, makundi madogo na kadhalika) Kupitia kwa mipango kama hii Wakristo hupata himizo la kukua katika kuelewa imani ya Ukristo na katika uhusiano baina yao na kwa Mungu. Tunaelewa uwanafunzi hujumlisha kujitolea katika kumtii Mungu na kuwa na nidhamu ya imani. Tunaamini kusaidiana ili kuishi maisha matakatifu, ushirika wa Wakristo na kuwajibikiana kwa mapendo. Wesley alisema, "Mungu alitupa watu wengine/wenza ili kuongezana nguvu."

Uanafunzi wa Ukristo ni njia ya maisha. Ni mfumo wa kujifunza jinsi Mungu angependa tuishi ulimwenguni. Tunapojifunza kuishi katika utiifu wa Neno la Mungu, kwa kujitolea kufuata nidhamu na kuwajibikiana, tunaanza kuelewa furaha ya kweli ya maisha ya kufuata nidhamu na maana ya uhuru wa Kikristo. Uwanafunzi sio jambo la ubinadamu, kujitolea kufuata amri na sharia. Ni njia ambayo Roho Mtakatifu mwishowe hutuwezesha kukua katika Kristo. Kwa njia ya uwanafunzi tunafanywa Wakristo wenye mwenendo mzuri. Lengo kuu la uwanafunzo ni kubadilishwa na kufanana na Yesu Kristo (2 Wakorintho 3:18)

Katika kusoma na kuomba maandiko, Wakristo hugundua chemi chemi ya viburudisho vya kumaliza kila kiu katika safari yao ya uwanafunzi. Haya hufanyika kwa kutiwa nguvu unapooshwa na Neno, unapoboreshwa na kuingia ndani ya Neno, kunywa ukweli wa Neno. Hapa wanafunzi wanagundua kwa furaha kuwa wanabadilishwa kwa kufanywa upya (akilini mwao) Warumi 12:2. Njia za Ukristo hufungua mbele ya macho zao kama vile barabara pana. Kwa usaidizi wa Mungu, wanaaanza kutembea kwenye barabara ya maisha, ambayo huonyesha maadili na tamaduni za wanadamu. Baada ya kupokea viburudisho

vya Neno, wanafunzi hujipata katika maisha ya huduma inayokua.

Tunathibitisha maadili ya kutoa maisha kwa nidhamu za kiroho katika kufunza wanawake na wanaume kuwa wanafunzi wa Kristo. Nidhamu kama vile maombi, mafundisho, kuwa pekee yako, huduma zote ni njia za kawaida za kuonyesha kujitolea katika maisha ya Ukristo.

Uwanafunzi unahitaji usaidizi na uwajibikaji kwa njia ya upendo. Kwa njia zetu binafsi, baadhi yetu watakuza nidhamu za kiroho ambazo huelekeza mtu kukua kiroho. Tunaamini kuwa tunafaa kuhimiza usaidizi ambao hupatikana kwa njia ya shule ya jumapili, makundi ya uwanafunzi, makundi ya mafundisho ya Biblia, mikutano ya maombi, makundi yanakushikilia katika uwajibikaji, Wakristo wanaokushauri kama inavyofaa katika kukua kiroho. Elewa sehemu ya uwajibikaji katika mikutano ya darasa la Wesleyani ambalo hutuhimiza kuishikilia na kuiweka mahala pake katika shirika la kisasa la Wakristo.

3d. Misheni Yetu Ya Elimu ya Juu Ya Ukristo

Tumejitolea katika elimu ya Ukristo ambapo waume kwa wake hutayarishwa kwa maisha ya huduma ya Ukristo. Katika seminari, vyuo vya Biblia, vyuo vya ushirika, na vyuo vikuu, tumejitolea katika kufuatilia ufahamu, na kuwakuza Wakristo wanaoheshimika na kuwatayarisha viongozi ili kutimiza wito tuliopewa na Mungu wa kuhudumu kanisani na ulimwenguni.

Elimu ya Juu ya Ukristo ni sehemu muhimu ya misheni ya Kanisa la mnazareti. Katika miaka ya kale ya

Kanisa la Mnazareti, vyuo vya elimu ya juu, vilianzishwa kwa madhumuni ya kutayarisha wanaume na wanawake wa Mungu kwa uongozi na huduma ya Ukristo ulimwenguni wa kuenenza huishaji wa Utakatifu kwa njia ya Uwesleyani. Baada ya miaka mingi ya kujitolea kwetu katika elimu ya juu ya Ukristo, tunazo sehemu nyingi za mafunzo ulimwenguni kote kama vile seminari, shule za Biblia, vyuo vya ushirika na vyuo vikuu.

Misheni yetu ya elimu ya juu ya Ukristo msingi wake ni maana ya kuwa watu wa Mungu. Tunapaswa kumpenda Mungu kwa, "roho, moyo na akili." Kwahivyo kuwa walinzi wema katika kukuza akili zetu, tunahitaji elimu na katika matumizi ya hekima yetu. Kwa sababu hii, tunajitolea kwa uwazi na uaminifu katika kukuza ufahamu na ukweli na pia kuziunganisha na Imani yetu ya Ukristo. Elimu ya juu ya Ukristo ni msingi wa maendeleo katika utawala wa akili zetu. Inapaswa kuwa sehemu ambapo kunao majadiliano na uvumbuzi wa ukweli na ufahamu wa Mungu na viumbe vyote vya Mungu.

Katika elimu ya juu ya Ukristo, imani haijatengwa, lakini imeunganishwa vyema kwasababu imani na mafundisho hukuzwa pamoja. Watu hukuzwa katika kila sehemu ya wazo nayo maisha hueleweka katika uhusiano wa kutamani na kuumbwa kama Mungu. Tabia za Wakristo na kuwatayarisha viongozi Wakristo kwa huduma kanisani na katika ulimwengu, zimetungwa katika sehemu ya kujifunza kuhusu Mungu, wanadamu na ulimwengu. Kutolea elimu ya juu ya Ukristo katika ubadilishaji wa mwanadamu ni muhimu katika maendeleo ya wanaume na wanawake Wakristo kwa uongozi wa umisheni kanisani na ulimwenguni.

Kama watu waliokolewa na kuitwa kuwa kama Kristo na kutumwa ili kuonyesha upendo wa Mungu ulimwenguni, tunashiriki na Mungu katika kazi ya kuwaokoa wanadamu. Elimu ya juu ya Ukristo huchangia sana katika kutufanya watu wa umisheni – kupeana kiwango kikubwa cha maarifa – na pia inafaa katika huduma ya Mungu katika wito wetu tofauti. Kushiriki kwetu kwa uaminifu katika kazi ya Mungu ya wokovu inahitaji tukuze wanaume na wanawake wa Mungu ambao wanaweza kuchukua mahali pao kama viongozi Wakristo kanisani na ulimwenguni.

Ulimwengu ambao tumeitwa kuhudumu unaendele kuungana na kuwa mgumu kila uchao. Kadri tunavyoendelea katika kazi kwa Ubwana wa Kristo na kushirikiana na Mungu katika kujenga Kanisa itaendelea kuhitaji kijitolea zaidi katika elimu ya juu ya Ukristo. ya kuendeleza wokovu kwa vizazi vya sasa na vile vijavyo, imani yetu ya ushuhuda.

Mwisho

Mwanzo wa karne ya 20, kanisa la mnazareti lilizaliwa! P.F. Bresse na wengineo walihukumika zaidi kuwa Mungu amewaita kwa nia ya kukiri Kanisa na neno la injili ya Yesu Kristo ulimwenguni katika tamaduni ya Utakatifu wa Uwesley. Kunazo alama ni za kweli katika dini hii. Kuanza na vuguvugu la vijana, Kanisa la Mnazareti linao zaidi wa washirika milioni 1.3 na linahubiri katika mataifa 119 ulimwenguni.

Ilipofika karne ya 21, siku za usoni za dini hii ziliendelea kung'aa! Wengi huamini dini hii haikuanzishwa

kwa ajili ya karne ya 20 ili ni kwa ajili ya karne ya 21. Tumewekwa sehemu nzuri ya kutoa mchango katika ulimwengu ujao. Msingi wa thibitisho hili ni katika urithi wa Utakatifu wa Uwesley ulio na msukumo wa matarajio wa mambo mazuri ya neema. Tunaamini kuwa hali ya wanadamu na jumuia kwa jumla yaweza kubadilshwa na neema ya Mungu. Tunayo imani katika ujumbe huu wa matumaini, unaofurika kutoka moyo wa Mungu Mtakatifu.

P.F Bresee alipenda kusema, "Jua halitui asubuhi." Bado ni asubuhi katika kanisa la mnazareti, na jua huwa halitui katika dini ye yote ulimwenguni. Tunao maratajio ya kuguza kwa vishindo karne ya 21 kwa ujumbe wa Utakatifu! Tunaona vyema, tumejitolea kikamilifu na imani iliyo imara. Tunaona karne ijayo kuwa fursa kuu ya kuwafanya wanafunzi wanaofanana na Kristo katika mataifa yote.

Maandiko yote yamenukuliwa katika Biblia Takatifu, (NIV) Haki miliki © 1973, 1978, 1984 na International Bible Society. Imetumiwa kwa idhini ya chumba cha uchapishaji cha Zondervan. Haki zote zimemilikiwa.